

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**



**TAARIFA KWA UMMA**

**WAKULIMA WA MIWA KAGERA WAASWA KUCHANGAMKIA SOKO LA MIWA  
KIWANDA CHA SUKARI KAGERA**

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Ashatu Kijaji, amewataka wakulima wa miwa wanaozunguka Kiwanda cha Sukari cha Kagera (Kagera Sugar) kuchangamkia soko la uhakika la zao hilo kwa kuongeza uzalishaji wa miwa kutokana na uhitaji mkubwa wa miwa kwa ajili ya uzalishaji wa miwa katika kiwanda hicho

Dkt. Kijaji alitoa wito huo baada ya kutembelea kiwanda hicho na kuelezwa kuwa katika msimu wa kilimo cha miwa uliopita wakulima wa miwa wanaozunguka kiwanda hicho walilipwa Shilingi bilioni 4 baada ya kukiuzia kiwanda hicho zaidi ya tani 56,000 za miwa.

Alisema kuwa bado mahitaji ya miwa kwa ajili ya kuzalisha sukari kiwandani hapo ni makubwa na kuwataka wakulima hao kupitia umoja wao wa wakulima wadogo wa miwa kuhamasishana kuongeza uzalishaji ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Kiwanda cha Sukari cha Kagera kimeendelea kuongeza uzalishaji tangu kipate wawekezaji ambapo uzalishaji huo umeongezeka kutoka tani 25,000 mwaka 2011/2012 hadi kufikia tani 75,000 na katika kipindi cha miaka mitano ijayo uzalishaji utafikia tani 170,000.

Afisa Mwendeshaji Mkuu wa Kiwanda hicho Bw. Ashwin Rana alisema wameanzisha Kitengo maalumu cha kuwaendeleza wakulima wadogo wa miwa wanaozunguka mashamba yao kwa kuendelea kuwapatia vitendeakazi ikiwemo matrekta, utaalumu pamoja na mbegu bora za miwa ili waweze kuchangia kuzalisha miwa yatakayosaidia waweze kufikia malengo yao ya kuongeza uzalishaji wa sukari.

Bw. Rana alisema kuwa tangu walipoanza kuunda umoja wa wakulima wadogo wa miwa wanaozunguka mashamba yao mwaka 2006, uzalishaji wao

umeongezeka kutoka tani 0 hadi tani 56,000 ambazo kiwanda hicho kilinunua msimu uliopita na kwamba wanatarajia uzalishaji wao utaongezeka zaidi.

“Mahitaji ya sukari nchini kwa mwaka ni tani 450,000 lakini uzalishaji uliopo hivi sasa ni tani 320,000 na kwa mikakati ya Kiwanda cha Sukari Kagera ya kuongeza mashamba na teknolojia ya uzalishaji wa bidhaa hiyo utapunguza kwa kiasi kikubwa upungufu huo” aliongeza Bw. Rana.

Kaimu Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania TRA Bw. Beatus Nchota, alieleza kuwa Mamlaka hiyo inapongeza jitihada kubwa ya kiwanda hicho kuongeza uzalishaji hatua ambayo itaongeza mauzo, ajira na hatimaye kuongeza kiwango cha kodi ambayo Kiwanda hicho kimekuwa kikilipa kwa kiwango kikubwa.

**Imetolewa na;**

**Benny Mwaipaja**  
**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**  
**Wizara ya Fedha na Mipango**